Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | August-2026

EAJK

# Malezi ya Mtoto wa Karne ya Ishirini na Moja Katika Novela za Assumpta K. Matei

**Authors**

**Eunice Wambui Mwaniki** [(1)]; **Joseph Nyehita Maitaria** [(2)]; **Erastus Mutahi Miricho** [(3)]

**Main author's email:** ewambui266@gmail.com

**(1.2.3) Karatina University, Kenya.**

**Cite this article in APA**

Mwaniki, E. W., Maitaria, J. N., & Miricho, E. M. (2026). Malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja katika novela za Assumpta K. Matei. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 5*(1), 125–133. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.1126

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2026.06.25
Accepted: 2026.07.24
Published: 2026.08.27

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Makala hii inachunguza namna malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja yanavyowasilishwa katika novela tatu za Assumpta K. Matei: *Mji wa Matarajio* (2022), *Uteuzi wa Chale* (2022) na *Tumaini la Mzeituni* (2025). Ingawa tafiti zilizotangulia zimejadili malezi, usawiri wa watoto, teknolojia na masuala ibuka katika fasihi ya watoto, bado hazijaeleza kwa kina namna mabadiliko ya kiuchumi, kiafya, kimazingira na kiteknolojia yanavyobadili mahitaji, majukumu ya walezi na mahusiano ya kimalezi katika novela za Matei. Utafiti ulitumia mkabala wa kiubora, muundo wa kimaelezo-kiuchanganuzi, usomaji wa karibu na uchanganuzi wa nyaraka. Data ilichanganuliwa kimaudhui kwa kuzingatia Nadharia ya Uhalisia wa Kijamii. Matokeo yanaonyesha kuwa umaskini katika *Mji wa Matarajio* unafanya elimu, ulinzi wa mtoto na msaada wa kihisia kuwa changamoto katika malezi; ugonjwa katika *Uteuzi wa Chale* unapanua wigo wa malezi kujumuisha afya, mwendelezo wa elimu, ustawi wa kihisia na ukuzaji wa kipaji; huku mafuriko katika *Tumaini la Mzeituni* yakifanya usalama, uhamaji, elimu na ustahimilivu kuwa sehemu muhimu za malezi. Aidha, sauti ya mtoto na ushirikiano wa familia, rika na taasisi huwezesha malezi kukidhi mahitaji yanayotokana na mazingira yanayobadilika. Utafiti unahitimisha kuwa Matei anawasilisha malezi kama mchakato shirikishi na jumuishi. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu unaonyesha namna fasihi ya watoto inavyoweza kuchangia malezi yanayozingatia haki, ustawi na mahitaji yanayobadilika ya mtoto wa karne ya ishirini na moja. Utafiti unapendekeza matumizi ya fasihi ya watoto katika kuhamasisha malezi yanayozingatia haki, ustawi na ujumuishaji.

**Maneno muhimu:** Fasihi ya watoto, malezi ya mtoto, mtoto wa karne ya ishirini na moja, ustawi wa kihisia.

**UTANGULIZI**

Malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja yanakabiliwa na changamoto zinazotokana na gharama za elimu, matatizo ya afya, teknolojia ya kidijitali, mabadiliko ya tabianchi, uhamaji na tofauti za kiuchumi. Hali hizi zinaifanya familia na jamii kuyaangalia malezi zaidi ya nidhamu na utiifu kwa kuyahusisha pia na ulinzi, elimu, afya, ustawi wa kihisia, usalama, ushirikishwaji na matumizi salama ya teknolojia (United Nations, 1989; UNICEF, 2017; UNICEF, 2021).

Katika makala hii, malezi yanaeleweka kama mchakato wa kumlinda na kumwezesha mtoto kukua kimwili, kielimu, kihisia, kijamii na kimaadili, huku akipewa mwongozo wa kukabiliana na mazingira yanayobadilika (Mwenda, 2020). Kwa mtazamo huu, malezi hayahusishi nasaha na nidhamu pekee, bali pia yanahusisha maamuzi ya kifamilia, mahusiano ya rika, msaada wa kihisia, elimu, afya, ukuzaji wa vipaji na ushirikiano wa taasisi zinazohusika na ustawi wa mtoto.

Katika makala hii, mtoto wa karne ya ishirini na moja anaeleweka kama anayekua katika mazingira yanayochanganya familia, shule, afya, uchumi, mazingira na teknolojia, huku akizidi kutambuliwa kama mwenye haki, sauti, hisia, ndoto na uwezo wa kushiriki katika maamuzi yanayomhusu (United Nations, 1989; Nodelman & Reimer, 2003). Mtazamo huu unatofautiana na ule unaomwona mtoto hasa kama mpokeaji wa maelekezo ya mtu mzima, kwa kuwa unasisitiza ushirikishwaji wa mtoto huku ukitambua kwamba ulinzi na rasilimali nyingi bado ziko chini ya watu wazima.

Mabadiliko katika mazingira ya mtoto huathiri malezi kwa njia mbalimbali. Changamoto za kiuchumi zinaweza kuzuia upatikanaji wa elimu na kuongeza hatari ya ajira ya mtoto; matatizo ya afya yanaweza kuvuruga masomo na ustawi wa kihisia; majanga ya kimazingira yanaweza kuathiri usalama, makazi na mwendelezo wa elimu; huku teknolojia ikipanua fursa za kujifunza na mawasiliano pamoja na kuhitaji mwongozo kuhusu matumizi yake, usalama na usawa wa upatikanaji (UNICEF, 2017; UNICEF, 2021). Hivyo, malezi ya mtoto wa sasa yanahitaji ushirikiano wa familia, rika, shule, huduma za afya na taasisi nyingine.

Novela tatu za Assumpta K. Matei zinafaa kwa uchunguzi huu kwa sababu zinaakisi mazingira tofauti lakini yanayokamilishana katika maisha ya mtoto wa karne ya ishirini na moja. *Mji wa Matarajio* unaonyesha uhusiano kati ya umaskini, elimu, ajira ya mtoto na mamlaka ya watu wazima; *Uteuzi wa Chale* unaunganisha afya, elimu, kipaji, urafiki na teknolojia; huku *Tumaini la Mzeituni* likiwasilisha mafuriko, uhamaji, usalama, elimu na matumizi ya teknolojia. Kwa pamoja, novela hizi zinamweka mtoto katika mazingira yanayohitaji maamuzi, ulinzi na msaada kutoka kwa familia, rika na taasisi.

Ingawa tafiti zilizopo zimejadili vipengele mbalimbali vya fasihi ya watoto na malezi, bado kuna pengo katika kuunganisha kwa pamoja mabadiliko ya kiuchumi, kiafya, kimazingira na kiteknolojia na namna yanavyobadili mahitaji ya mtoto, majukumu ya walezi, ustawi wa kihisia, sauti ya mtoto na mahusiano ya mamlaka katika novela za Assumpta K. Matei. Makala hii inalenga kuziba pengo hilo kwa kuchanganua namna *Mji wa Matarajio*, *Uteuzi wa Chale* na *Tumaini la Mzeituni* zinavyowasilisha malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja katika elimu na uchumi, afya na ustawi wa kihisia, mazingira na uhamaji, teknolojia, pamoja na sauti, haki, ujumuishaji na mtandao wa malezi.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Fasihi ya watoto huchukuliwa kama matini zinazozingatia tajriba, lugha na mahitaji ya mtoto, hivyo huwa na nafasi katika namna jamii inavyomwelewa na kumlea mtoto (Hunt, 1994). Mtazamo huu unaifanya fasihi ya watoto kuwa zaidi ya chombo cha burudani au mafunzo ya maadili; inaweza pia kufichua changamoto za maisha ya mtoto na mahusiano yake na familia, shule na jamii. Nodelman na Reimer (2003) wanaonyesha kuwa fasihi ya watoto hujengwa katika mvutano wa mamlaka kati ya mtoto na mtu mzima kwa sababu watu wazima hushiriki katika uandishi, uchapishaji, uteuzi na usomaji wa matini hizi. Mtazamo huu ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu unatoa msingi wa kuchunguza malezi kwa kuangalia iwapo mtoto anawasilishwa kama mpokeaji wa maamuzi ya watu wazima au kama mshiriki mwenye sauti, haki na uwezo wa kushiriki katika maisha yake. Hivyo, fasihi ya watoto inatoa eneo mwafaka la kuchanganua malezi kama uhusiano unaohusisha mtoto na walezi wake.

Katika tafiti za Kiafrika na hasa Kenya, Muthubi (2005) alichunguza mikakati na mbinu za usimilishwaji katika fasihi ya watoto na kuonyesha umuhimu wa kuzingatia hadhira ya watoto katika uchaguzi wa lugha na muundo wa matini. Mchango huu unaweka msingi wa kuzingatia mahitaji na tajriba ya mtoto katika uchanganuzi wa matini, ingawa utafiti huo ulijikita katika usimilishwaji badala ya malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja. Mwenda (2020), kwa upande mwingine, alichunguza taswira ya malezi na kubainisha nafasi ya familia, maadili na mahusiano ya kijamii katika ujenzi wa mtoto. Utafiti wake unaonyesha kuwa malezi yanaweza kuchanganuliwa kupitia matendo, mazungumzo na migogoro ya wahusika. Hata hivyo, mtazamo huo haujitoshelezi kueleza malezi katika mazingira ambayo afya, teknolojia, mazingira, uhamaji na ustawi wa kihisia vinabadilisha mahitaji ya mtoto. Utafiti huu unaendeleza michango hii kwa kuangalia malezi kama mchakato unaohusisha familia pamoja na rika, shule, wataalamu na taasisi nyingine.

Suala la haki, sauti na ushirikishwaji wa mtoto linaendelea kupanua mjadala wa malezi. Miricho na Mbuthia (2017) walionyesha umuhimu wa namna watoto wanavyosawiriwa katika hadithi za Kiswahili na namna usawiri huo unavyoweza kuathiri mtazamo wa mtoto kuhusu nafsi yake na ulimwengu unaomzunguka. Miricho (2021) naye alionyesha kuwa fasihi ya watoto ya karne ya ishirini na moja imepanuka na kujumuisha haki za watoto, afya, ujumuishaji, ajira ya mtoto, mazingira na teknolojia. Michango hii inaonyesha kuwa mtoto wa sasa anahitaji kuchanganuliwa kama mhusika mwenye mahitaji na haki mbalimbali, lakini tafiti hizo hazikuunganisha kwa kina sauti ya mtoto, ustawi wa kihisia, malezi ya rika na mgawanyo wa mamlaka kati ya mtoto na walezi katika novela za Matei. Utafiti huu unachukua msingi huo na kuuchanganya na suala la malezi ili kuchunguza namna sauti ya mtoto inavyoshirikiana na wajibu na mamlaka ya walezi.

Mazingira ya kijamii, kiuchumi na kimazingira pia yanaathiri namna malezi yanavyotekelezwa. Kairu (2005) alichunguza uhalisi na mtindo katika fasihi ya watoto na kubainisha umuhimu wa mazingira, wahusika na migogoro inayounganisha matini na maisha halisi ya mtoto. Karanja (2008) naye alionyesha namna fasihi ya watoto inavyoweza kuakisi masuala ibuka ya kipindi inamoandikwa. Tafiti hizi zinaunga mkono mtazamo kwamba maisha ya mtoto hayawezi kutenganishwa na mazingira yanayomzunguka. Hata hivyo, hazikulenga novela za Assumpta K. Matei wala kuunganisha kwa pamoja umaskini, afya, mazingira, teknolojia na mahitaji ya malezi. Kwa hiyo, utafiti huu unaendeleza msingi huo kwa kuchunguza namna mabadiliko ya mazingira yanavyobadili majukumu ya walezi, usalama wa mtoto, upatikanaji wa elimu na ustawi wake.

Teknolojia imeongeza mazingira mapya katika malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja. Gatwiri (2015) alichunguza hadithi za watoto katika mtandao na kuonyesha umuhimu wa mtandao katika mazingira ya usomaji na mawasiliano ya mtoto. Mchango huu unaonyesha kuwa teknolojia imepanua namna mtoto anavyopata na kushiriki maarifa. Hata hivyo, katika muktadha wa malezi, matumizi ya teknolojia yanahitaji kuhusishwa pia na mwongozo, usalama, maadili na usawa wa upatikanaji wa rasilimali. Utafiti huu unapanua mjadala wa Gatwiri kwa kuangalia teknolojia si kama chombo cha mawasiliano pekee, bali kama sehemu ya malezi ya kidijitali inayohitaji ushiriki wa walezi na taasisi katika kumsaidia mtoto kuitumia kwa manufaa ya kujifunza, mawasiliano na maendeleo yake.

Kwa mtazamo wa kimataifa, *Convention on the Rights of the Child* inaweka msingi wa kumtambua mtoto kama mwenye haki ya ulinzi, maendeleo na kushirikishwa katika mambo yanayomhusu (United Nations, 1989). Mtazamo huu unaimarisha hoja kwamba malezi ya kisasa hayawezi kutegemea utiifu pekee, bali yanapaswa pia kumtambua mtoto kama mshiriki katika maisha yake. Katika mazingira ya kidijitali, UNICEF (2017) inaonyesha mabadiliko yanayoletwa na teknolojia katika maisha ya watoto, wakati UNICEF (2021) inaonyesha namna mabadiliko ya tabianchi yanavyoweza kuathiri haki na ustawi wa mtoto. Mitazamo hii ya kimataifa inaongeza upana wa mjadala unaojitokeza katika tafiti za Kiafrika na Kenya, ambazo zimejadili malezi, usawiri wa mtoto, mazingira, afya na teknolojia. Muunganiko wa mitazamo hiyo unaonyesha kuwa malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja yanahitaji kuangalia kwa pamoja haki, usalama, ustawi wa kihisia, mazingira, teknolojia na uwezo wa walezi kuitikia mahitaji yanayobadilika.

Kwa msingi wa mapitio haya, tafiti zilizopo zimechangia kuelewa vipengele mbalimbali vya fasihi ya watoto na malezi, lakini zimejikita zaidi katika maeneo maalumu kama usimilishwaji, uhalisi na mtindo, masuala ibuka, matumizi ya mtandao, taswira ya malezi au usawiri wa watoto. Bado kuna pengo katika uchambuzi unaoviunganisha vipengele hivyo na kuchunguza namna mabadiliko ya kiuchumi, kiafya, kimazingira na kiteknolojia yanavyobadili mahitaji ya mtoto, majukumu ya walezi, ustawi wa kihisia, sauti na mahusiano ya mamlaka katika novela za Assumpta K. Matei. Utafiti huu unajaza pengo hilo kwa kuchanganua *Mji wa Matarajio*, *Uteuzi wa Chale* na *Tumaini la Mzeituni* kama matini zinazowasilisha malezi katika mazingira tofauti ya maisha ya mtoto wa karne ya ishirini na moja. Kwa kufanya hivyo, utafiti unaunganisha mitazamo ya kimataifa na Kiafrika na kuonyesha namna elimu na uchumi, afya na ustawi wa kihisia, mazingira na uhamaji, teknolojia, sauti na haki, pamoja na mtandao wa malezi vinavyoshirikiana katika kujenga tajriba ya mtoto wa sasa.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kiubora na muundo wa kimaelezo-kiuchanganuzi kwa kuwa data yake ilikuwa ya kimaandishi na ilihitaji kufasiriwa kwa kuzingatia wahusika, matukio, mazungumzo, mandhari na mahusiano ya kijamii. Usampulishaji wa kimakusudi ulitumika kuteua novela tatu za Assumpta K. Matei: *Mji wa Matarajio* (2022), *Uteuzi wa Chale* (2022) na *Tumaini la Mzeituni* (2025). Novela hizi tatu zilitosha kwa sababu, kwa pamoja, zinaakisi mazingira tofauti lakini yanayokamilishana ya mtoto wa karne ya ishirini na moja, yakiwamo changamoto za kiuchumi na elimu, afya na ukuzaji wa kipaji, pamoja na mazingira, uhamaji, usalama na teknolojia. Sampuli hiyo haikulenga kuwakilisha fasihi yote ya watoto ya Kiswahili, bali kutoa data ya kina inayolenga suala la malezi katika kazi teule za Matei. Data ilikusanywa kwa usomaji wa karibu na uchanganuzi wa nyaraka. Dondoo, matukio, mazungumzo, wahusika na maelezo ya mandhari yenye uhusiano na malengo ya utafiti yalitambuliwa, kurekodiwa pamoja na namba za kurasa na kupewa misimbo kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kabla ya uchanganuzi ili kupunguza upendeleo. Data ilichanganuliwa kimaudhui kwa kuongozwa na Nadharia ya Uhalisia wa Kijamii na kulinganisha ruwaza ndani na baina ya novela. Uhalali uliimarishwa kwa kuhusisha data na malengo ya utafiti na kulinganisha matini tatu, huku uaminifu ukihakikishwa kwa usomaji wa mara kadhaa, matumizi ya mfumo mmoja wa misimbo na kuhifadhi dondoo pamoja na marejeo ya kurasa.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Sehemu hii inawasilisha matokeo kuhusu namna malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja yanavyojengwa katika *Mji wa Matarajio*, *Uteuzi wa Chale* na *Tumaini la Mzeituni*. Matokeo hayachukulii changamoto za mtoto kama mada zilizojitenga; yanaonyesha namna changamoto hizo zinavyobadili mahitaji ya mtoto na namna wazazi, walezi, rika, shule, wataalamu na jamii wanavyoweza kumlinda, kumsikiliza, kumwelekeza na kumwezesha. Matokeo yamepangwa katika maeneo ya elimu na uchumi; afya, hisia na kipaji; mazingira na uhamaji; teknolojia; pamoja na sauti, ujumuishaji na mtandao wa malezi.

**Malezi, Elimu na Mabadiliko ya Kiuchumi**

Katika *Mji wa Matarajio*, hali ya kiuchumi ya familia inaathiri moja kwa moja elimu na mustakabali wa mtoto. Herina anamaliza shule ya msingi akiwa na matarajio ya kuendelea na masomo, lakini mama yake anamweleza:

"Sitamudu kukukidhia mahitaji ya kujiunga na hiyo shule ya bweni" (Matei, 2022a, uk. 2).

Kauli hii inaonyesha tofauti kati ya kutambua umuhimu wa elimu na kuwa na uwezo wa kuigharamia. Mama yake Herina anatamani binti yake aendelee na masomo, lakini ukosefu wa fedha unazuia utekelezaji wa azma hiyo. Hivyo, malezi hayawezi kutegemea upendo na nia njema pekee; yanahitaji rasilimali zinazomwezesha mlezi kutekeleza wajibu wa kumlinda na kumwandaa mtoto. Katika muktadha huu, changamoto ya kiuchumi inaweka mlezi katika uchaguzi mgumu kati ya mahitaji ya familia ya sasa na haki ya mtoto ya elimu.

Suluhisho linalopendekezwa ni kumpeleka Herina mjini kuajiriwa katika kazi ya kumlea mtoto wa mwajiri. Hatua hiyo inabadilisha nafasi yake kutoka mtoto anayehitaji malezi na elimu kuwa mlezi wa mtoto mwingine. Hali hii inafichua tofauti za kitabaka, ambapo mtoto wa familia maskini anakosa masomo ili kutoa huduma katika familia yenye uwezo zaidi. Herina anatambua athari za mpango huo anapouliza:

"Kwa nini anataka kuniingiza kwenye ajira, mtoto mdogo kama mimi?" (Matei, 2022a, uk. 2).

Swali hili linaonyesha kuwa Herina anaelewa umri wake, haki yake ya elimu na umuhimu wa kushirikishwa katika maamuzi yanayoathiri maisha yake. Upinzani wake hautokani na uvivu, bali ufahamu kwamba ajira ya mapema inaweza kukatiza masomo na kupunguza nafasi zake za baadaye.

Umaskini pia unamwathiri Herina kihisia. Analazimika kuficha hofu yake ili asimtie mama yake mashakani, ingawa hana uhakika kuhusu kazi, makazi na maisha yake ya baadaye. Matokeo haya yanaonyesha kuwa maamuzi ya kiuchumi yanaweza kumfanya mtoto kubeba mzigo wa kihisia unaozidi umri wake. Malezi bora yanahitaji, kwa hiyo, kulinda elimu ya mtoto na pia kumpa maelezo, faraja na usalama wa kihisia.

Mwisho wa novela, Daktari Jemima anatambua madhara ya ajira hiyo na kusaidia kurejesha elimu ya Herina. Hatua hiyo inaonyesha nafasi ya mtu mzima katika kurekebisha uamuzi unaomdhuru mtoto na inaonyesha kuwa malezi yanaweza kuimarishwa na mtandao wa watu wazima pale familia inaposhindwa kutimiza wajibu wake kwa sababu ya mazingira. Hata hivyo, utegemezi wa msaada wa mtu mmoja unaonyesha udhaifu wa mifumo ya ulinzi wa mtoto na elimu. Kwa hiyo, malezi yenye mafanikio yanahitaji si nia ya mlezi pekee bali pia mifumo inayomsaidia mlezi kulinda haki za mtoto.

Matokeo haya yanaafikiana kwa kiasi na Mwenda (2020), ambaye alibainisha umuhimu wa familia, maadili na mahusiano ya kijamii katika malezi ya mtoto. Hata hivyo, novela ya Matei inaonyesha kwa uwazi zaidi kwamba familia inaweza kuwa na nia njema ya kumlea mtoto lakini ikashindwa kutekeleza wajibu huo kutokana na ukosefu wa rasilimali. Kwa upande mwingine, Kairu (2005) anaonyesha umuhimu wa mazingira na migogoro inayotambulika katika kuunganisha fasihi ya watoto na maisha halisi ya mtoto. *Mji wa Matarajio* unaendeleza mtazamo huu kwa kuonyesha namna umaskini wa familia unavyogeuka kuwa kikwazo cha elimu na chanzo cha mzigo wa kihisia. Tofauti kuu ni kwamba utafiti huu unaunganisha mazingira hayo ya kiuchumi na suala la haki ya elimu, sauti ya mtoto na ustawi wa kihisia.

**Afya, Ustawi wa Kihisia na Ukuzaji wa Kipaji**

Katika *Uteuzi wa Chale*, malezi yanaonekana katika kutambua na kukuza kipaji cha mtoto. Chale ana ndoto ya kuwa mtangazaji, lakini mazingira yake hayana studio wala vifaa vya kitaalamu. Anatumia rasilimali zilizopo:

"Angeketi juu ya jiwe ambalo aliliita 'Sanduku la Mtangazaji' na kuanza kutangaza" (Matei, 2022b, uk. 3–4).

Kugeuza jiwe kuwa "Sanduku la Mtangazaji" kunaonyesha ubunifu na uwezo wa mtoto kujifunza katika mazingira yenye rasilimali chache. Chale pia anatumia redio ya baba yake kusikiliza watangazaji na kujifunza mbinu zao. Redio inakuwa darasa lisilo rasmi linalomsaidia kukuza lugha, ujasiri na utambulisho wake.

Juhudi za Chale zinaonyesha kuwa mtoto anaweza kuanzisha safari ya kukuza kipaji chake, lakini anahitaji kupewa mwongozo, kutambuliwa na kupewa fursa na watu wazima pamoja na taasisi. Malezi, hivyo, hayahusu kumrekebisha mtoto anapokosea pekee; yanajumuisha pia kutambua uwezo wake, kuupa nafasi ya kukua na kumsaidia kuutumia kwa njia yenye manufaa.

Ugonjwa unapojitokeza, mahitaji ya Chale yanabadilika. Anaondolewa shuleni na katika kundi la marika na kulazwa hospitalini. Wasiwasi wake unaonekana anaposema:

"Huko nyumbani wenzangu wanaendelea kusoma. Sijui kama nitawahi kuwafikia" (Matei, 2022b, uk. 40).

Kauli hii inaonyesha kuwa ugonjwa haumwathiri kimwili pekee. Unamletea hofu ya kubaki nyuma katika masomo, kupoteza mawasiliano na marafiki na kukatizwa kwa ndoto yake. Malezi ya mtoto mgonjwa yanahitaji, kwa hiyo, matibabu pamoja na msaada wa kihisia, maelezo yanayoeleweka na mpango wa kuendeleza ujifunzaji. Hapa jukumu la mlezi linapanuka kutoka kumpeleka mtoto kupata matibabu hadi kuhakikisha kuwa ugonjwa hauondoi kabisa nafasi yake ya elimu, mahusiano na ukuaji wa kipaji.

Hospitali inakuwa sehemu ya mtandao wa malezi kwa sababu namna wataalamu wanavyowasiliana na mtoto inaweza kupunguza au kuongeza hofu yake. Chale hawezi kufafanuliwa kwa ugonjwa pekee; bado ni mwanafunzi, rafiki na mtoto mwenye kipaji. Matokeo

yanaonyesha kuwa malezi jumuishi yanapaswa kuunganisha afya, elimu, hisia na maendeleo ya kipaji.

Matokeo haya yanaendeleza hoja ya Mwenda (2020) kwamba mahusiano ya kijamii ni sehemu muhimu ya ujenzi wa mtoto, lakini yanaipanua kwa kuonyesha kwamba afya inaweza kuvuruga mahusiano hayo na mwendelezo wa elimu. Pia yanaendana na Miricho (2021), ambaye anaonyesha upanuzi wa fasihi ya watoto ya karne ya ishirini na moja katika kushughulikia afya na mahitaji mapya ya mtoto. Hata hivyo, *Uteuzi wa Chale* unaonyesha kwa undani zaidi uhusiano wa afya, hisia, elimu na kipaji katika mchakato mmoja wa malezi.

**Mazingira, Uhamaji na Ustahimilivu**

Katika *Tumaini la Mzeituni*, malezi yanajengwa katika mazingira ya mafuriko yanayotishia nyumba, biashara, elimu na usalama wa familia. Wazazi wa Heri na Tana wanalazimika kuamua iwapo wabaki katika mazingira waliyozoea au wahame kwa ajili ya usalama. Olivia anasema:

"La muhimu zaidi ni usalama... Tumeiwazia elimu yenu" (Matei, 2025, uk. 17).

Kauli hii inaonyesha kuwa uamuzi wa kuhama unazingatia usalama wa mwili pamoja na mwendelezo wa elimu. Watoto wanaelezwa sababu za uamuzi na kupewa nafasi ya kuuliza maswali. Ingawa mamlaka ya mwisho yanabaki kwa wazazi, Heri na Tana wanatambuliwa kama watu wenye hisia na matarajio yatakayoathiriwa na mabadiliko hayo. Hivyo, malezi yanayofaa katika mazingira ya janga yanahitaji mlezi kufanya maamuzi ya kulinda mtoto huku akizingatia pia sauti, elimu na ustawi wake wa kihisia.

Hali hii inatofautiana na ya Herina, ambaye anakutana na mpango uliokamilika kuhusu ajira yake. Tofauti hiyo inaonyesha kuwa malezi shirikishi hayamaanishi kumpa mtoto mamlaka yote, bali kumpa taarifa, kusikiliza maoni yake na kueleza namna maslahi yake yalivyozingatiwa.

Uhamaji una athari za kihisia kwa sababu mtoto anaweza kuacha marafiki, shule na mazingira aliyoyazoea. Kwa hiyo, usalama wa mwili unahitaji kuambatana na maandalizi ya kihisia na msaada wa kuzoea mazingira mapya. Heri anaendelea kushikilia ndoto yake baada ya uhamaji, jambo linaloonyesha ustahimilivu. Hata hivyo, ustahimilivu haupaswi kueleweka kama kumwacha mtoto avumilie changamoto peke yake. Unapaswa kujengwa kupitia mawasiliano, msaada na mazingira yanayomwezesha kuendelea na maisha.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa malezi katika mazingira ya majanga yanahitaji kuunganisha usalama, elimu na ustawi wa kihisia. Familia inaweza kufanya maamuzi ya haraka, lakini ulinzi mpana wa mtoto unahitaji pia mifumo ya taarifa, makazi salama na huduma zinazolinda mwendelezo wa masomo.

Matokeo haya yanaunga mkono hoja ya Karanja (2008) kwamba fasihi ya watoto huakisi masuala-ibuka ya kipindi inamoandikwa. Mafuriko na uhamaji katika *Tumaini la Mzeituni* yanaonyesha namna changamoto za kimazingira zinavyoweza kuingia moja kwa moja katika malezi na maisha ya mtoto. Vilevile, yanaendeleza mtazamo wa Miricho (2021) kwamba mazingira ni miongoni mwa masuala muhimu katika fasihi ya watoto ya karne ya ishirini na moja. Utafiti huu unaongeza kwamba mazingira hayapaswi kuchukuliwa kama mandhari tu; yanaathiri maamuzi ya kifamilia, usalama, elimu, mahusiano na ustawi wa kihisia wa mtoto.

**Teknolojia na Malezi ya Kidijitali**

Teknolojia katika novela teule inabadilisha namna mtoto anavyojifunza, kukuza kipaji na kuwasiliana. Chale anatumia redio kujifunza utangazaji, huku Tana akitumia mtandao kufanya utafiti. Katika *Tumaini la Mzeituni*, Tana anajikumbusha:

"Sharti uamke kufanya utafiti kwenye mtandao kabla akina Heri hawajaamka kuleta msongamano" (Matei, 2025, uk. 11).

Kauli hii inaonyesha mtoto anayepanga muda na kutumia mtandao kama chanzo cha maarifa. Hata hivyo, "msongamano" unaonyesha kuwa muunganisho unashirikiwa na kwamba upatikanaji wa maarifa unategemea muda, ubora wa huduma na idadi ya watumiaji. Hivyo, kuwa na kifaa au mtandao hakumaanishi kuwa kila mtoto ana fursa sawa ya kujifunza.

Malezi ya kidijitali yanapaswa kumwezesha mtoto kutumia teknolojia kwa manufaa huku akipewa mwongozo kuhusu muda, faragha, usalama na

uaminifu wa taarifa. Hivyo, jukumu la mlezi halipaswi kuwa kumzuia mtoto kutumia teknolojia pekee, bali kumjengea uwezo wa kuitumia kwa uwajibikaji. Novela zinaonyesha zaidi manufaa ya teknolojia kuliko hatari zake, kama taarifa potovu, matumizi ya teknolojia kupita kiasi na athari kwa usingizi au mahusiano ya kijamii. Hili ni eneo linalohitaji kupewa nafasi zaidi katika fasihi ya watoto wa karne ya ishirini na moja.

Usawa wa kidijitali unahitaji pia kuzingatia watoto wasiokuwa na vifaa, umeme, data au mtu wa kuwaelekeza. Teknolojia inapaswa kuwa nyenzo ya kupanua elimu, si chanzo kipya cha tofauti kati ya watoto. Malezi ya sasa yanahitaji, kwa hiyo, uwiano kati ya upatikanaji, usalama, maadili na matumizi yenye kusudi.

Matokeo haya yanaendana na Gatwiri (2015), ambaye alionyesha kuwa mtandao umeunda mazingira mapya ya usomaji na mawasiliano kwa mtoto. Hata hivyo, *Tumaini la Mzeituni* linaonyesha zaidi ya uwepo wa teknolojia kwa kuibua suala la upatikanaji usio sawa wa rasilimali za kidijitali. Hali ya "msongamano" inaonyesha kwamba mtoto anaweza kuwa na nia na uwezo wa kujifunza lakini akakabiliwa na vikwazo vya kimazingira na kifamilia. Kwa hiyo, utafiti huu unaongeza katika mjadala wa Gatwiri (2015) kwa kuhusisha matumizi ya teknolojia na wajibu wa malezi, usawa wa fursa na mwongozo wa mtoto katika matumizi ya kidijitali.

**Sauti, Ujumuishaji na Mtandao wa Malezi**

Kwa kulinganisha novela hizo, watoto wana uwezo wa kueleza mahitaji yao, lakini rasilimali na mamlaka ya mwisho hubaki kwa watu wazima. Herina anaeleza hofu yake kuhusu ajira, Chale anaonyesha wasiwasi kuhusu afya na masomo, huku Heri na Tana wakishiriki katika mazungumzo kuhusu uhamaji. Hivyo, watoto hawajengwi kama wapokeaji wasio na ufahamu, bali kama wahusika wanaoweza kufikiri, kuuliza na kutoa maoni.

Hata hivyo, sauti pekee haiwapi uwezo wa kubadili hali zao. Herina hawezi kujilipia shule, Chale hawezi kuamua matibabu yake, nao Heri na Tana hawawezi kudhibiti mafuriko. Malezi shirikishi yanahitaji, kwa hiyo, kutumia mamlaka ya watu wazima kwa uwajibikaji: kutoa taarifa inayoeleweka, kusikiliza maoni ya mtoto na kufanya maamuzi yanayolinda maslahi yake. Hivyo, kusikiliza mtoto hakumaanishi kuondoa mamlaka ya mlezi; kunamaanisha kutumia mamlaka hayo kwa namna inayomwezesha mtoto kushiriki na kufaidika na uamuzi unaomhusu.

Familia si taasisi pekee inayoshiriki katika malezi. Katika *Uteuzi wa Chale*, vijana wa Bwawa la Mpingoni wanabadilishana mawazo, habari na maadili. Marika pia wanatambua kipaji cha Chale na kumpa hadhira ya kwanza. Malezi ya rika yanaweza kujenga kujiamini, mawasiliano na hali ya kukubalika, lakini hayawezi kuchukua nafasi ya familia, shule na taasisi katika kutoa elimu, matibabu, vifaa na ulinzi.

Katika novela zote tatu, mtandao wa malezi unajumuisha familia, marika, shule, waajiri, hospitali na jamii. Uwepo wa wahusika hawa hauhakikishi malezi bora; ubora wa malezi hayo hutegemea mawasiliano, maadili, rasilimali na uwajibikaji. Familia inaweza kuwa na upendo lakini ikakosa fedha, marika wanaweza kutoa msaada lakini wakahitaji mwongozo, na taasisi zinaweza kuwa na wataalamu lakini zikahitaji mifumo inayohakikisha huduma inamfikia mtoto. Kwa hiyo, malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja yanaonekana kama jukumu la pamoja linalohitaji ushirikiano wa walezi na taasisi mbalimbali.

Ujumuishaji unahitaji kutambua mahitaji tofauti ya Watoto. Herina anahitaji kulindwa katika haki yake ya elimu na dhidi ya ajira ya mapema; Chale anahitaji matibabu, msaada wa kihisia na mwendelezo wa kipaji; Heri na Tana wanahitaji usalama na msaada wa kuzoea uhamaji. Usawa, kwa hiyo, haumaanishi kuwapa watoto wote msaada unaofanana, bali kuwapa msaada unaolingana na mazingira na mahitaji yao.

Kwa jumla, novela teule zinaonyesha kuwa malezi yanahitaji kuzingatia mazingira mahsusi ya mtoto na kuunganisha uwezo wake na uwajibikaji wa familia, rika na taasisi. Hata hivyo, utegemezi wa suluhisho kwa watu binafsi unapunguza ukosoaji wa mifumo mipana inayozalisha changamoto za watoto.

Matokeo haya yanaafikiana na Nodelman na Reimer (2003), ambao wanaonyesha umuhimu wa mvutano wa mamlaka kati ya mtoto na mtu mzima katika fasihi ya watoto. Katika novela hizi, mtoto ana sauti lakini mamlaka ya mwisho mara nyingi hubaki kwa watu wazima. Hata hivyo, matokeo yanaonyesha kwamba

mamlaka hiyo inaweza kutumika kumzuia mtoto au kumlinda na kumwezesha. Vilevile, matokeo yanaendeleza hoja ya Miricho na Mbuthia (2017) kuhusu umuhimu wa usawiri wa mtoto kwa kuonyesha mtoto kama mhusika mwenye hisia, mawazo, ndoto na uwezo wa kutoa maoni.

Kwa kulinganisha matokeo ya sehemu zote, umaskini katika *Mji wa Matarajio* unaonyesha kuwa malezi yanahusisha ulinzi wa haki ya elimu na kupunguza mzigo wa kihisia; ugonjwa katika *Uteuzi wa Chale* unaonyesha kuwa malezi jumuishi yanahitaji kuunganisha huduma ya afya, elimu, hisia na kipaji; na mafuriko katika *Tumaini la Mzeituni* yanaonyesha kuwa malezi yanahitaji usalama, mawasiliano ya kifamilia, mwendelezo wa elimu na ustahimilivu. Teknolojia inaongeza mahitaji ya mwongozo wa kidijitali, huku sauti na ujumuishaji zikihitaji mamlaka ya watu wazima itumike kwa uwajibikaji. Kwa pamoja, matokeo haya yanaonyesha kuwa malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja yanafanikiwa pale walezi na taasisi wanapounganisha ulinzi, usikilizaji, mwongozo, rasilimali na fursa za maendeleo ya mtoto. Matokeo haya yanaendeleza hoja ya Mwenda (2020) kuhusu mtandao wa mahusiano katika malezi, Kairu (2005) na Karanja (2008) kuhusu uhusiano wa fasihi na mazingira halisi ya mtoto, Gatwiri (2015) kuhusu mazingira ya kidijitali, na Miricho (2021) pamoja na Miricho na Mbuthia (2017) kuhusu upanuzi wa masuala na usawiri wa mtoto katika fasihi. Mchango wa makala hii ni kuonyesha jinsi vipengele hivyo vinavyoungana katika dhana moja ya malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho**: Kwa ujumla, novela za Assumpta K. Matei zinawasilisha malezi ya mtoto wa karne ya ishirini na moja kama mchakato shirikishi unaounganisha elimu, hali ya kiuchumi, afya, ustawi wa kihisia, ukuzaji wa kipaji, mazingira, usalama, teknolojia, haki na sauti ya mtoto. Katika *Mji wa Matarajio*, changamoto ya kiuchumi inafanya malezi yahusishe ulinzi wa elimu na kuzuia ajira ya mtoto; katika *Uteuzi wa Chale*, afya inaonyesha umuhimu wa kuunganisha matibabu, elimu, hisia na kipaji; na katika *Tumaini la Mzeituni*, mafuriko yanafanya usalama, uhamaji, elimu na ustahimilivu kuwa sehemu muhimu za malezi. Kwa pamoja, novela hizi zinaonyesha kuwa mtoto ana haki na sauti, lakini mafanikio ya malezi yanategemea uwezo wa walezi na taasisi kumlinda, kumsikiliza, kumwelekeza na kumpa fursa za maendeleo.

**Mapendekezo**: Wazazi, walezi na walimu waimarishe mawasiliano na ushirikishwaji wa watoto katika maamuzi yanayowahusu. Taasisi za elimu, afya na ulinzi wa mtoto ziimarishe mifumo ya kulinda elimu, afya na usalama wakati wa changamoto za kiuchumi na majanga. Waandishi wa fasihi ya watoto waendeleze usawiri wa mtoto mwenye sauti, haki na mahitaji yanayobadilika, huku tafiti zijazo zikichunguza mapokezi ya matini hizi miongoni mwa watoto wenyewe.

## MAREJELEO


Gatwiri, J. N. (2015). *Tathmini ya hadithi za watoto katika mtandao* [Master's thesis, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository. https://ir-library.ku.ac.ke/items/f7307a98-5d57-464b-98cd-42f16485859f

Hunt, P. (1994). *An introduction to children's literature*. Oxford University Press.

Kairu, W. M. (2005). *Uhalisi na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto* [Master's thesis, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository. https://ir-library.ku.ac.ke/items/cfea69e6-fd72-45ed-830c-2bc0a71d87a3

Karanja, D. W. (2008). *Usawiri wa maswala-ibuka katika hadithi za watoto* [Master's thesis, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository. https://ir-library.ku.ac.ke/items/2c0a33ac-e8ba-4ae7-8068-2437104aac86

Lukács, G. (1963). *The meaning of contemporary realism* (J. & N. Mander, Trans.). Merlin Press.

Matei, A. K. (2022a). *Mji wa matarajio*. One Planet Publishing & Media Services Limited.

Matei, A. K. (2022b). *Uteuzi wa Chale*. One Planet Publishing & Media Services Limited.

Matei, A. K. (2025). *Tumaini la Mzeituni*. Newton Educational Resources Limited.

Miricho, E. M. (2021). *Ukiushi wa kanoni katika hadithi teule za watoto za John Kobia na Wadi Wamitila* [Tasnifu ya uzamivu, Chuo Kikuu cha Laikipia].

Miricho, M., & Mbuthia, E. M. (2017). The impact of the depiction of children in selected Swahili children stories. *International Journal of Contemporary Applied Sciences,* 4(1), 9–20. https://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/163751

Muthubi, F. M. (2005). *Mikakati na mbinu za usimilishwaji katika fasihi ya watoto* [Master's thesis, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository. https://ir-library.ku.ac.ke/items/a159a5c2-3f76-4558-bdef-a539cfdfd22c

Mwenda, A. K. (2020). *Taswira ya malezi ya watoto katika riwaya za Tumaini (2006) na Dunia Mashaka Makuu (2004)* [Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta]. Kenyatta University Institutional Repository. https://ir-library.ku.ac.ke/items/b5e87094-9adc-4af4-9045-bc335f156eaa

Nodelman, P., & Reimer, M. (2003). *The pleasures of children's literature* (3rd ed.). Allyn and Bacon.

UNICEF. (2017). *The state of the world's children 2017: Children in a digital world*. UNICEF. https://www.unicef.org/reports/state-worlds-children-2017

UNICEF. (2021). *The climate crisis is a child rights crisis: Introducing the Children's Climate Risk Index*. UNICEF. https://www.unicef.org/reports/climate-crisis-child-rights-crisis

United Nations. (1989). *Convention on the Rights of the Child*. United Nations. https://www.ohchr.org/en/instruments-mechanisms/instruments/convention-rights-child

Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.